**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA_MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo mkunjufu kabisa, kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na weledi wa hali ya juu kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kulipeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa kushiriki vyema kazi ya kupitia mapendekezo ya Bajeti yaliyowasilishwa kwenye Kamati jambo linalonipa mimi wepesi wa kuiongoza Kamati hii. Aidha, wajumbe walionesha umakini na umahiri katika kutoa michango yao yenye lengo la kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo, biashara na utalii zinaimarika na kuziletea nchi yetu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue fursa hii niwatambue wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Azza January Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Abdulgulam Hussein | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 8. | Ndg. Mwaka Mwinyi Wazir | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati hii ya Kilimo, Biashara na Utalii ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha, kama Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ilivyoelekeza. Hivyo, Kamati katika kufanikisha jukumu hili ilikutana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, maliasili na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati napenda kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, maoni yetu kuhusiana na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kuzingatia program kuu tano (5) zinazotekelezwa na Wizara na ambazo utekelezaji wake umejikita katika Programu ndogo sita (6).

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,** Katika Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo, Kamati imebaini changamoto katika Wakala wa Serikali wa Matrekta na Zana za Kilimo ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 Wakala imetengewa kukusanya kiasi cha Tzsh Milioni 100, ambapo Kamati ilielezwa kuwa, mapato hayo yanatakiwa kuwasilishwa moja kwa moja hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, mapato haya yanatokana na michango ya wananchi wanaochangia katika kuburugiwa mashamba yao, fedha ambayo hapo awali wakulima hawa walikuwa wakilipa Halmashauri na kwa sasa italipwa moja kwa moja Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala ipo kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi, hivyo endapo mapato haya yatapelekwa moja kwa moja hazina yanaweza kuleta usumbufu wa kuchelewa kuwapatia huduma wananchi hawa hasa ukizingatia Wakala imeundwa kisheria. Sheria No.2 ya mwaka 2019 iliyounda

Wakala huu haijatoa mamlaka haya. Kufanya hivyo ni kukiuka Sheria na taratibu tulizozipanga wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhika juu ya suala la mapato haya kwenda hazina, kamati inahisi si busara kwa sababu Wakala haitakuwa na kianzio chengine cha mapato hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa upatikanaji wa huduma kwa wakulima hao hasa ukizingatia kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa letu na waswahili wanasema '***Kilimo hakimtupi mtu***'

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hii Kamati inaishauri Serikali kuandaa mfumo maalumu utakaorahisisha matumizi ya fedha hizi zinazokusanywa kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wananchi wake katika kupata huduma muhimu kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Matrekta na zana za kilimo ina majukumu makubwa ya kuhakikisha kuwa inawapa huduma bora wananchoi wa visiwa vyote viwili, jambo la kusikitisha ni kuona kuwa kwa upande wa kisiwa cha Pemba Wakala huu una matrekta mabovu ambayo hayatoi huduma yoyote kwa wananchi. Kupitia maoni haya ya Kamati nkuhusiana na bajeti hii tunaiomba Serikali ifanye utaratibu wa kuhakikisha kuwa bajeti hii tunayoipitisha inatenga fedha maalum kwa ajili ya matengenezo ya matrekta yale.

**Mheshimiwa Spikaa,** Changamoto nyengine iliyobainika kwa upande wa Matumizi ya Wizara kupitia Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo, chini ya mwamvuli wa program yake ndogo ya kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji ni kuondolewa kwa huduma kadhaa ambazo zingeweza kusaidia utekelezaji mzuri wa Programu hii. Miongoni mwa huduma zilizoondolewa ni pamoja na huduma ya Matengenezo ya Visima na Pampu, huduma ya Kutoa Mafunzo ya Mbinu Bora za Umwagiliaji Maji, huduma ya Matengezo ya Mitaro ya Umwagiliaji Maji, huduma ya Kuboresha Usimamizi wa Maendeleo ya Miundombinu ya Umwagiliaji Maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitika kuona huduma zote hizi zimeondolewa na kujiuliza maswali mengi, ni kwa jinsi gani Programu hii itaweza kutekelezwa kwa ufanisi kwa mwaka huu wa fedha?

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inashauri kurudishwa kwa huduma zote muhimu ndani ya Programu hii kwa lengo la kusaidia kufikia malengo yaliyopangwa. Kamati inaiona huduma ya Kutoa Mafunzo ya Mbinu Bora za Umwagiliaji Maji ipewe kipaumbele na irudishwe ndani ya Programu hii

kutokana na umuhimu wake. Elimu ndio msingi wa maendeleo kwa kila jambo, wakulima wanapaswa kupatiwa elimu juu ya mbinu bora za umwagiliaji Maji lengo ni kuleta tija katika kilimo chao.

**Mheshimiwa Spika,** Kama tujuavyo, Umwagiliaji Maji unatumia fedha nyingi, Kamati inaishauri Wizara kufanya tafiti katika umwagiliaji wa mazao mengine ya matunda badala ya kujikita katika umwagiliaji wa zao la mpunga pekee, hili litaweza kusaidia katika kunyanyua uchumi na kuboresha afya za wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa umwagiliaji maji katia bonde la Mlemele na Makwararani kazi zake zinaonekana kusua sua kutokana na ukweli kwamba fedha nyingi za utekelezaji wa mradi huu, zimetoka lakini mradi haujakamilika. Kamati inatoa msisitizo wa kukamilishwa mradi huu kwa wakati kutokana na ukweli tunaoupata katika usemi wa Kiswahili usemao '**Chelewa chelewa utakuta mwana si wako**'. Tunatumia msemo huu kwa kumaanisha kwamba mradi huu umetumia fedha nyingi sana na matokeo yaliyokusudiwa kwa ukamilifu wake hadi sasa hayajaonekana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu, kwa uwamuzi wake wa kuwapatia wananchi miche ya mikarafuu na miche ya mazao ya mtunda bure bila ya wananchi hao kulipia fedha ya aina yoyote. Hatua hii ya Serikali inawapa muamko na hamasa kubwa wananchi kujikita katika kilimo cha mazao hayo na kuwakwamua kiuchumi na kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza mkazo zaidi uwekze katika uoteshaji wa miche ya mikarafuu ili kuongeza uzalishaji wa zao hili hasa tukizingatia kuwa zao la karafuu ni miongoni mwa vianzio vikuu vya uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati inasikitika sana kutokana na hali iliyoikuta wakati ilipofanya ziara zake katika baadhi ya vitalu vya kuotesha miche ya mikarafuu na mazao ya matunda ksiwani Pemba. Kamati ilikutana na changamoto ya baadhi ya wafanyakazi kutolipwa stahiki zao kama sheria ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza. Wafanyakazi hawa wamejitoa sana kiasi kwamba sisi Kamati tunaamini kuwa walikua wakijitoa ilimradi tu **'Punda afe mzigo wa bwana ufike'.**

**Mheshimiuwa Spika**, Kamati haikuridhika na hali hiyo kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wafanyakazi hao wengine wamefanya kazi muda mrefu bila ya kwenda likizo na bila ya kupatiwa stahiki zao. Hali hii inasitikisha sana hasa tukizingatia kuwa, wafanyakazi hawa wameamua kujitoa kwa hali na mali kwa lengo la kusiadia nchi yao.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hali hii, Kamati pia imebaini kuwepo hali ya muingiliano mkubwa wa Programu usiokuwa na uwiano katika utaoji na utekelezaji wa majukumu katika taasisi husika. Kuna baadhi ya Programu zinaonekana kumezwa ndani ya Programu nyengine, hali ambayo kwa uoni wa Kamati haiwezi kuleta tija katika utoaji wa huduma zilizopangwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha kumezwa kwa baadhi ya Programu ndani ya Programu nyengine ni kuzishushia hadhi yake hasa ukizingatia Programu hizo zimeundwa kwa mujibu wa Sheria. Mfano mzuri ni Wakala wa Huduma za Matrekta imeshushwa na kuwa ni mtoa huduma, suala hili Kamati inaliona haliko rafiki.

**Mheshimiwa Spika,** ili kulifanyia kazi suala hili Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipago kuliangalia upya suala la kubebanisha Programu ndani ya Programu nyengine lengo ni kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa kila taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba pia nichukue nafasi hii nielezee suala zima la upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wetu. Suala hili limekua na changamoto kubwa katika upatilkanaji wake. Kamati imebaini kuwa wakulima walio wengi kwa Unguja na Pemba wanakosa mbolea kwa wakati kwa ajili ya kuoteshea mazao yao. Tunaiomba Wizara kupitia bajeti hii, ihakikishe kuwa inachukua hatua madhubuti na kuhakikisha suala hili linapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kunsusru mazao ya wakulima wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka uliopita program hii ilitengewa shilingi **Bilioni sabiini na tisa, Milioni thelathini , laki saba na na tisini na mbili alfu (79,030,792,000)** ambapo kwa mwaka huu wa 2021/2022 Programu hii imetengewa shilingi **Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia mbili na Ishirini na saba Laki tatu na elfu nne** (**37,227,304,000)** ambapo fedha hizi zimepungua ukilinganisha na fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka jana. Kamati imesikitishwa na kiwango hicho cha fedha ambacho ni kidogo ukilinganisha na majukumu makubwa ya program hii. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kupatikana

kwa fedha hizo kwa wakati ili malengo yaliyopangwa kwa mwaka huu yaweze kutimizwa kwa wakati.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu**,** mashamba ya Serikali viumbe hai pamoja na mazingira yao.

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetengewa kutumia **Tsh. Bilioni Mbili, Milioni mia nane na hamsini na tisa, laki nane na kumi na tano alfu** (**2,859,815,000**) kupitia huduma zake mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 fedha ambayo inaonekana kupungua sana kutoka **Tsh Bilioni tano, Milioni mia nane arobaini na sita, laki sita na arobaini na Nane alfu (5.846,648,000)** kwa mwaka wa fedha ulioishia mwezi Juni 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kama tujuavyo kwamba Wizara ya Kilimo ina Misitu mingi ya hifadhi ikiwemo Msitu wa hifadhi wa Ngezi, Msitu wa Hifadhi Jozani ambayo inaweza kuwa ni vivutio vizuri kwa watalii wa ndani na wa nje. Suala la kupungua kwa kiwango hiki cha fedha kunaweza kuzorotesha uhifadhi na uendelezwaji wa misitu hii hali inayoweza kurudisha nyuma juhudi za kuiletea maendeleo Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Msitu wa Ngezi, Kamati ilipofanya ziara katika maeneo hayo ilitembelea jengo jipya lililojengwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi pamoja na shughuli nyengine. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na ujenzi wa jengo lile kutoakana na kasoro mbali mbali zilizopo ikiwemo kasoro ya nyufa katika jengo ambalo hata halijaanza kutumika, kukosekana kwa huduma ya umeme, huduma ambayo imeelezwa kuwa gharama zake ni kubwa sana. Kamati inashauri kupitia bajeti hii jengo lile liwekewe umeme pamoja na hudma zote muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Kamati za wana vijiji walizoziunda kwa lengo la kuilinda na kuihifidhi misitu hiyo, Kamati ilielezwa kuwa kuna asilimia ya fedha ambayo wanavijiji hao hupatiwa kutokana na miradi iliyopo na juhudi zao za kuihifadhi misitu hiyo. Kamati imebaini kuwa fedha hizo haziwafikii walengwa moja kwa moja na badala yake ni watu wachache tu wanaonufaika na fedha hizo. Hali hii inawarudisha nyuma wana kijiji hao katika juhudi zao za kujitolea katika kuilinda misitu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia hatuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Kamati inaomba jumuiya hizo upatikanaji wa stahiki zao ufanywe kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Kamati tunaamini maana ya usemi usemao **'Hala hala jirani kuliko ndugu aliyembali** '. Kamati inayasema haya kutokana na ukweli kwamba, jumuiya zilizoundwa katika vijiji vinavyozunguka misitu yetu ndizo zilizoko karibu na misitu yenyewe, hivyo si rahisi kwa jumuiya hizi kuweza kuhujumu misitu yetu na badala yake tukifanya vyenginevyo kwa kutowalipa ile asilimia iliyokubalika kwa pande zote athari kubwa inaweza kupatikana katika ulinzi wa misitu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia hotuba hii ya maoni ya kamati kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya kilimo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara hii kuufanya Msitu wa Jamii wa Micheweni wakati umefika sasa Msitu huu tuufanye uwe ni Msitu wa Hifadhi kutokana na ukubwa wake. Pia tunaiomba Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya umuhimu wa Msitu huu kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kadhia hii, Kamati inaishauri Serikali kutafuta mbinu bora za uingizaji wa fedha kwa Programu zetu kwa kuzitengea programu fedha kwa mujibu wa mahitaji yao kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu waliyojipangia.

**Mheshimwa Spika,** Kamati iliangaza vyema huduma ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uekezaji wa Miradi ya jamii katika Sekta ya Misitu Kifungu **HL01020104**, ilibaini kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa fedha iliyotengwa katika utekelezaji wa huduma hii muhimu. Kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha **TSh. Milioni Themanini, Laki mbili na Tisiini alfu (80,290,000)** zimetengwa kutumika katika kutekeleza huduma hii, fedha ambayo Kamati inaona kwamba haitaweza kutekeleza azma na malengo waliojipangia ukilinganisha na fedha waliyotengewa mwaka 2020/2021 iliyofikia kiasi cha **Tsh. Milioni Mia Sita thelathini na nane, Laki tano na thelathini na tisa alfu (638,539,000.)**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka huu wa 2021/2022 program hii imetengewa jumla ya shilingi **Bilioni mbili, Milioni mia nane hamsini na tisa, laki nane na kumi na tano alfu 2,859,815,000** fedha ambazo ni kidogo ukilinganisha na fedha za bajeti ya mwaka uliopita wa 2020/2021 ambazo zilikuwa ni shilingi **Bilioni Tano, Milioni Mia Nane arobaini na Sita, Laki Sita na Arobaini na Nane Alfu** (**5,846,648,000**.)

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hii Kamati inaiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mara nyengine, kukaa na kuliangalia upya suala la utengaji wa fedha huku wakizingatia utekelezaji halisi wa huduma zilizopangwa kupitia Programu busika, hii itaweza kusaidia utekelezaji mwema wa yale yote yaliyopangwa kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo ina lengo la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu kuu hii kupitia Programu yake ndogo ya Uzalishaji na Utabibu wa Mifugo bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa Mtambo wa kuzalishia gesi ya kupandishia ng'ombe wa sindano, hali inayopelekea kiwango kidogo cha uzalishaji wa gesi jambo linalowagharimu wafugaji wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kukamilisha taratibu za manunuzi ya mtambo mpya kwa lengo la kuwaondolea wafugaji usumbufu wanaoupata hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa hivi karibuni kumezuka maradhi ya mifugo ikiwemo ng'ombe, kuku na aina nyengine za ndege, maradhi ambayo yanaweza kuhatarisha afya za watumiaji wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hii Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara yake ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuzitekeleza vyema huduma za Kinga na Udhibiti wa Maradhi ya Mifugo ili kusudi tuweze kunusuru uingiaji wa maradhi ya mifugo nchini na kuziweka afya za wananchi wetu katika hali ya usalama zaidi hasa ukizingatia wananchi wengi ni watumiaji wazuri wa malighafi hizi toka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa huduma zinazotolewa katika mifugo bado ziko nyuma, hivyo Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Mifugo kuhakikisha inatoa huduma zilizo bora zaidi kwa wafugaji wetu juu ya mifugo yao ili waweze kuikinga na maradhi hatarishi ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini changamoto katika Programu ndogo ya Utabibu wa Mifugo, kwa mwaka huu wa fedha haikutengewa fedha yoyote

wakati kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2021 Huduma hii ilitengewa jumla ya **Tsh Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na kumi saba, Laki, Nane na Kumi na Tano Alfu (1,417,815,000.)**

**Mheshimiwa Spika** , Kamati haijaridhika kuiona hali hii na kuishauri Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango kuliangalia tena suala hili hasa tukizingatia hali hii inaweza kurudisha nyuma kasi ya maendeleo kwa wafugaji wetu kwa vile watakosa huduma za kinga na udhibiti wa maradhi kwa mifugo yao**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka huu wa 2021/2022 program hii imetengewa jumla ya **shilingi Bilioni Sita, Milioni mia Sita themanini, Laki Sita na kumi na Sita Alfu** (**6,680,616,000)** fedha ambazo zimeongezeka ukilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita ambapo program hii ilitengewa shilingi **Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Themanini na Nane, Laki Tisa na tisiini Alfu (3,688,990,000)**. Kwa ongezeko hili Kamati inachukua nafasi hii kupongeza na inaiomba Serikali kuhakikisha kuwa fedha hizi zinapatikana kwa wakati ili malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika program hii yaweze kufikiwa.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo, Kamati inasikitishwa na kiwango kidogo cha kasma iliyopangiwa Programu hii. Kwa mwaka huu wa fedha Progamu imepangiwa **Tsh Bilioni Sita, Milioni Mia Tisa thelathini na Sba, na Elfu Kumi na Nane.(6,937,018,000)** kutoka **Bilion**i **Kumi na Nne, Milioni Mia mbili sitiini na Saba, Laki mbili na Elfu Nane** (**14,267,208,000)** kwa mwaka wa fedha uliokwisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na kadhia hii Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kutekeleza yale majukumu ambayo itaweza kuyatekeleza kutokana na kasma iliyopangiwa Programu hii. Aidha Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo ijitahidi kusimamia na kutekeleza yale yaliyo muhimu ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato pamoja na kuzitumia kwa uangalifu fedha zilizotengwa kwa lengo la kujinyanyua kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaisisitiza Wizara kufanya tafiti mbalimbali zitakazoweza kusimamia utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ili kuweza kupiga hatua ya maendeleo. Kwa upande wa suala la mafunzo Kamati inaishauri Wizara kuiwachia Serikali kuu hasa ukizingatia bajeti ndogo iliyopangiwa haitoweza kukidhi mahitaji ya kuwasomesha watendaji wake.

**HITIMISHO**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati , pamoja na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kumega wakati wao na kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikiwasilisha hutuba hii. Sasa wakati umefika niwaombe wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimaye waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale yote waliyojipangia katika mwaka huu wa fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika**, Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

……………………………

**Azza Januari Joseph.**

**Makamo Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii**

**Baraza la Wawakilishi**

**Zanzibar.**